

# **Historia na Maendeleo ya Kiswahili Nchini Zimbabwe**

Edwell Dzomba  
Chuo Kikuu cha Zimbabwe

## **Ikisiri**

Nchini Zimbabwe Kiswahili kilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe mwezi Agosti, mwaka 2013. Tofauti na nchi za Afrika Mashariki, hadi sasa katika karne hii ya ishirini na moja, Kiswahili hakijaenea sana katika nchi za Kusini mwa Afrika. Kutambulishwa kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe ni mojawapo ya ishara za maendeleo ya Kiswahili katika sehemu ya Kusini mwa Afrika. Makala hii inalenga kueleza historia na maendeleo ya Kiswahili nchini Zimbabwe. Lengo kuu ni kuchunguza hali ya Kiswahili nchini Zimbabwe kwa kuangalia maendeleo yake kabla na baada ya kutambulishwa kwa masomo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Hoja yetu kuu ni kwamba, kutambulishwa kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe haikuwa chanzo cha kuwapo kwa Kiswahili nchini Zimbabwe. Kiswahili kilikuwa kinatumika katika nyanja mbalimbali lakini ufundishaji ndio ulikuwa haujaanzishwa rasmi. Tumejadili chachu mbalimbali ambazo tunaweza kusema kwamba zinaendelea kusukuma mbele maendeleo ya Kiswahili nchini Zimbabwe, kwa mfano, teknolojia, mavazi, sanaa na biashara, kwa kutaja chache tu. Chachu hizi zimejadiliwa katika kuangalia jinsi zinavyochangia katika kueneza Kiswahili nchini Zimbabwe. Tumehitimisha kwa kuangalia kwamba ni kitu gani kifanyike ili kukikua Kiswahili nchini Zimbabwe kuwa lugha ya umajumui ya kuwaunganisha Wazimbabwe na watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa ujumla.

## **1.0 Utangulizi**

Makala hii inachunguza historia na maendeleo ya Kiswahili nchini Zimbabwe kwa kuangalia maendeleo yake kabla na baada ya kuanzishwa kwa kozi za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe mwaka 2013. Kuna nadharia mbalimbali kuhusiana na asili au chimbuko la Kiswahili ingawa siyo madhumuni ya makala hii kujadili nadharia hizi. Wataalamu mbalimbali (taz. Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Nurse na Spear, 1985; Mazrui na Shariff, 1994; Massamba, 2002 na 2008; kwa kutaja wachache) wameonesha mitazamo tofautitofauti kuhusiana na historia ya Kiswahili. Ni wazi kwamba Kiswahili kimekuwa mojawapo ya lugha ambazo huchaguliwa na watu wengi katika ukanda wa Afrika Mashariki na nchi jirani (Moshi, 2006). Kwa mujibu wa Mukuthuria (2006), katika karne nyingi zilizopita Kiswahili kilikuwa lugha ya Afrika Mashariki tu na baada ya karne ya kumi na

nane kilianza kusambaa sehemu tofautitofauti duniani. Mukuthuria anaendelea kusema kwamba katika karne ya ishirini Kiswahili kilichukua hatua kubwa katika nchi za Afrika Mashariki ambapo nchi kama Tanzania na Kenya zilianza kutumia lugha hii katika nyanja mbalimbali za kiutawala. Tofauti na Kiingereza, Kiswahili tangu karne za awali ni lugha ambayo haikuwa na ubaguzi kwa misingi ya dini na rangi. Wataalamu wengine wanalinganisha asili ya utamaduni wa Waswahili na dini ya Kiislamu, lakini kwa ujumla tunaweza kusema kuwa Kiswahili kilitengeneza utamaduni mmoja na kuwaunganisha Waafrika, Waarabu na Wahindi kutokana na chakula chao, namna wanavyofanya shughuli mbalimbali, na mavazi yao (Moshi, 2006).

Katika karne hii ya ishirini na moja, Kiswahili ni lugha ambayo tunaweza kuiona katika mabara mbalimbali duniani, kwa mfano, Amerika ya Kusini na Kaskazini, Asia na Ulaya. Kwa hiyo, Kiswahili ni mojawapo ya lugha ambazo zimeshika kasi sana kimaendeleo duniani. Hali ya Kiswahili Zimbabwe tunaweza kuielezea kwa kuangalia Kiswahili kama mojawapo ya lugha zinazoendelea kwa kasi duniani. Ingawa kuna vikwazo katika harakati za kukiendeleza Kiswahili nchini Zimbabwe; ni wazi kwamba Kiswahili ni lugha ambayo imeshapiga hatua na kutambulika kama lugha ya kigeni inayoweza kutumika katika nyanja mbalimbali.

### **1.1 Historia ya Kiswahili nchini Zimbabwe kabla ya Kutambulishwa Rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe**

Kabla ya kutambulishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe mwaka 2013, Kiswahili kilikuwa kinatumika katika nyanja mbalimbali nchini humo. Kwa namna moja au nyingine, Wazimbabwe walikuwa wanakitumia na bado wanakitumia Kiswahili bila kujua au kwa kujua kuwa lugha wanayoitumia ni Kiswahili. Jambo hili tunaweza kuliona katika makanisa ya Kipentekoste. Makanisa hayo, mathalani, Zimbabwe Assemblies of God Africa (ZAOGA) ambalo nchini Tanzania linajulikana kama Foward in Faith Ministries (FIF), na Apostolic Faith Mission (AFM), nyimbo za Kiswahili zimekuwa zikitumika kabla ya Kiswahili kutambulishwa rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Siyo jambo la ajabu kuona huduma mbalimbali zitolewazo na makanisa tajwa, kama vile ibada na nyimbo, zikitumia Kiswahili. Ni jambo la kawaida kwa sasa kuwasikia waumini wakiimba nyimbo zinazobeba maneno kama *Yesu ni wami (wa mimi) wa uzima wa milele* au *Nitamwambia bwana, kwa kuwa yeye ameniona*. Hizi ni nyimbo ambazo zimekuwa zikitumika kwa muda mrefu katika jamii za makanisa haya. Kadhalika, vituo vya televisheni kama Ezekiel TV cha Kanisa la ZAOGA kimekuwa kikirusha nyimbo za Kiswahili kwa muda mrefu kabla ya Kiswahili kutambulishwa rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe.

Aidha, kuna baadhi ya nyimbo za wanamuziki wa Kiswahili ambazo zimekuwa maarufu sana katika nchi ya Zimbabwe. Wimbo wa Les Wanyika unaoitwa *Sina Makosa*, ulikuwa maarufu katika nchi ya Zimbabwe kabla ya

ufundishaji rasmi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Kwa mfano, Radio Zimbabwe na National FM (Radio ya Taifa) zimekuwa zikirusha nyimbo hizi katika vipindi mbalimbali. Siku hizi siyo jambo la kushangaza kusikia mtu akiimba wimbo huu bila kujua kuwa lugha anayotumia ni Kiswahili.

Katika utamaduni wa Waswahili kuna mavazi kama fulana na khanga ambayo hutumika kufikisha jumbe tofautitofauti kwa wanajamii. Kwa mujibu wa Timammy na Swaleh (2016:1), “ulimwengu wa khanga au lesa ni ulimwengu wa uzuri, rangi za kupendeza, nakshi changamano, mavazi ya kusitiri na papo hapo kupitisha ujumbe fulani kupitia methali na misemo.” Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa vazi hili limevutia na linaendelea kuwavutia wageni wanaotembelea nchi za Afrika Mashariki, wakiwamo Wazimbabwe. Kwa hiyo, wageni wanaotembelea nchi kama Tanzania na Kenya hununua fulana zinazobeba maneno kama *Karibu Zanzibar* au *Hakuna Matata*. Kabla ya kutambulishwa rasmi kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe, kuna baadhi ya maduka ya mavazi nchini Zimbabwe yalikuwa yanauza mavazi haya. Ni jambo la kawaida kukutana na mtu katika nchi ya Zimbabwe akiwa amevaa fulana iliyoandikwa *Hakuna Matata* na ukimwuliza maana yake kwa Kiingereza anaweza kukusomea maandishi hayo vizuri kabisa lakini bila kujua kuwa lugha hiyo ni Kiswahili.

Kwa mujibu wa Karangwa (2006), uhuru wa nchi ya Msumbiji ulipatikana baada ya vita na wapigania uhuru wa FRELIMO wengi wao walipata mafunzo ya kijeshi nchini Tanzania. Anaendelea kusema kwamba hakuna ushahidi kama Kiswahili kilitumika baadaye katika kampeni zao. Karangwa (2006) hakutaja nchi kama Zimbabwe lakini ni dhahiri kwamba wapigania uhuru wa Zimbabwe walishirikiana kwa kiasi kikubwa na majeshi ya Msumbiji katika kipindi cha vita vya kupigania uhuru nchini Zimbabwe. Aidha, katika juhudi za kushirikiana katika kupinga ukoloni kuna baadhi ya wanajeshi kutoka Zimbabwe walikuwa na kambi zao katika nchi ya Tanzania. Baada ya Zimbabwe kupata uhuru wanajeshi hawa walirudi Zimbabwe na walikuwa wanajua baadhi ya sentensi na maneno ya Kiswahili. Jambo hili linathibitishwa na Kezilahabi (2003) akijadili kuhusu utunzi wa ushairi wa Kiswahili anaposema, “Sioni kwa nini mpigania uhuru wa Zimbabwe na ajuaye Kiswahili asipewe fursa ya kuandika ushairi wake bila vina kwa kuogopeshwa na maneno kama: “Kiswahili kina wenyewe”, “Waswahili hasa” wakati mwingine “Waswahili haswa haswa”. Ingawa Kezilahabi alikuwa anaonesha kuwa utunzi wa ushairi wa Kiswahili hauna kikomo na vilevile kuna uwezekano wa Wazimbabwe kuchangia katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili, ni dhahiri kuwa wanajeshi hawa walileta Kiswahili nchini Zimbabwe kabla ya kutambulishwa rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe.

Akiunga mkono hoja ya kuwapo kwa Kiswahili nchini Zimbabwe kutokana na wapigania uhuru walioishi nchini Tanzania, Mulokozi (2003) anasema kwamba mwaka 1988 alipata nafasi ya kutembelea nchi ya Zimbabwe na aliona duka moja limeandikwa jina ‘Nyama Choma’. Alipoingia dukani, mwenye duka akamuuliza, “Wewe unatoka Tanzania?” akamjibu, “Ndiyo ninatoka Tanzania.” Akasema

nimekutambua kwa lafudhi ya Kiingereza chako. Baada ya hapo mwenye duka alimwelezea kwamba yeye alikuwa mwanajeshi na aliwahi kuishi Tanzania katika kambi ya Nachingwea katika kipindi cha vita vya kupigania uhuru. Tangu hapo wakaanza kuzungumza kwa Kiswahili. Kutokana na maelezo haya tunaona kwamba kabla ya kutambulishwa rasmi Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe kilikuwapo nchini humo.

Kuna baadhi ya wanajeshi waliojiunga na sanaa ya muziki na wakaanza kutunga nyimbo zao kwa Kiswahili. Kundi la wanamuziki linaloitwa Kasongo Band ambalo lilikuwa likiongozwa na Ketai Muchawaya lilianzishwa na wanajeshi wapigania uhuru wa Zimbabwe. Wanajeshi hawa walikuwa wanatoka kundi la National Liberation Army (ZANLA) na walikuwa pamoja na Dhembo Kenyatta, Rex Moto Moto, Stalin Organ, Fainos Mapurisa, Jack Ncube na Marko Sibanda. Baada ya Zimbabwe kupata uhuru mwaka 1980, Kasongo Band walitoa nyimbo mbalimbali ambazo zilikuwa na Kiswahili ndani yake. Nyimbo hizi ni kama “Mapambano Makali”, “Sisi Wakuu”, “Kiongozi Wasekela” na “Asante Sana”. Katika wimbo wa “Asante Sana”, Kasongo Band walikuwa wanawashukuru viongozi wa nchi mbalimbali, kwa mfano, Samora Machel wa Msumbiji na Julius Nyerere wa Tanzania kwa kuwasaidia kupata uhuru wa Zimbabwe. Nyimbo hizi zilikuwa zinarushwa sana katika vituo mbalimbali vya redio nchini Zimbabwe.

Pia, kujenga usalama na kuulinda ni mojawapo ya jukumu muhimu la nchi za Kiafrika. Mwaka 1998, Zimbabwe ilituma wanajeshi ili washiriki katika kujenga usalama katika vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Wanajeshi hawa waliporudi baadhi yao walikuwa wanaongea Kiswahili chenye lafudhi ya Kikongo. Hili ni jambo linaloonesha kuwa Kiswahili nchini Zimbabwe kilikuwa kimeshaingia kabla ya kutambulishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba kuanzishwa rasmi kwa kozi za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe hakukuwa chanzo cha kutumika kwa Kiswahili nchini Zimbabwe. Hii ilikuwa ni moja kati ya juhudi za kukiendeleza nchini humo kupitia ufundishaji rasmi.

## **1.2 Kutambulishwa Rasmi kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe**

Katika nchi ya Zimbabwe Kiswahili kilikuwa hakijawahi kufundishwa rasmi kabla ya mwaka 2013. Watu waliokuwa na uwezo wa kuongea Kiswahili ni wanajeshi ambao waliishi Afrika Mashariki wakati wa harakati za kupigania uhuru na wafanyabiashara wachache wanaotembelea nchi kama Tanzania na Kenya mara kwa mara. Mwaka 2013 nchi ya Zimbabwe iliimarisha mchakato wa kuendeleza lugha za Kiafrika. Kiswahili pamoja na Kitonga<sup>1</sup> ni lugha mbili zilizoanza kufundishwa rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi. Mwezi Agosti mwaka 2013, Chuo Kikuu cha Zimbabwe

---

<sup>1</sup> Lugha ya Kibantu inayozungumzwa kusini na magharibi mwa nchi ya Zambia, kaskazini mwa nchi ya Zimbabwe na sehemu chache katika nchi ya Msumbiji.

kilianza kufundisha digrii ya Kiswahili katika Shahada ya Sanaa Tumizi (*Bachelor of Applied Arts*) katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi. Wanafunzi waliosajili kusoma kozi hii walikuwa themanini na watano. Darasa hili liliendelea mpaka mwaka 2015 ambapo wanafunzi walitakiwa wachague kozi mbili tu katika mwaka wa mwisho. Baadhi ya wanafunzi waliacha kozi ya Kiswahili na wakabaki ishirini tu. Hao ishirini ndio waliohitimu kama wanafunzi wa kwanza wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe mwaka 2016.

Kupitia makubaliano kati ya Chuo Kikuu cha Zimbabwe na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, walimu waliokuwa wanafundisha Kiswahili walikuwa wanatoka katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Walimu hao waanzilishi ni Gordian Katikiro na Titus Mpemba. Mwaka 2016, mwalimu Katikiro aliaga dunia na akaacha pengo kubwa katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Zimbabwe. Mwaka huohuo, Mwalimu Leonard Herman Bakize kutoka TATAKI alifika ili kujaza nafasi iliyoachwa na marehemu Katikiro na ufundishaji wa Kiswahili ukasonga mbele. Katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi, lugha za Kiafrika zinazofundishwa ni Kitonga, Kiswahili, Kindebele na Kishona. Mbali na kufundisha Kiswahili katika madarasa ya kawaida, Idara iliamua kuanzisha Masomo ya Cheti cha Kiswahili (*Kiswahili for Beginners Certificate*) ambapo watu wasio wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zimbabwe wanapata fursa ya kujifunza Kiswahili na kupata cheti baada ya miezi mitatu. Katika miaka ya 2018 na 2019 kumejitokeza maendeleo makubwa kutokana na idadi ya wanafunzi takribani thelathini, waliojisajili katika kozi ya Masomo ya Cheti cha Kiswahili (*Kiswahili for Beginners*) kila semesta.

Pia, mwaka 2016 kupitia makubaliano baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Zimbabwe, wanafunzi watatu<sup>2</sup> waliohitimu shahada ya kwanza wakihusisha masomo ya Kiswahili katika shahada zao, waliteuliwa kwenda kusoma shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hatua hii ilichukuliwa kutokana na juhudi za kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Zimbabwe. Wanafunzi hao walipomaliza masomo yao walirudi kuendeleza ufundishaji wa Kiswahili kama walimu wa Kiswahili katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi, Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Mkakati huu pia ulilenga kuwafanya Wazimbabwe wenyewe wafundishane Kiswahili baada ya waasisi kutoka Tanzania kumaliza mikataba yao. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kuanzishwa kwa Kiswahili nchini Zimbabwe siyo jambo la Zimbabwe tu bali hata nchi za Afrika Mashariki zinachangia katika kukikuza Kiswahili. Jambo hili linathibitishwa na nchi kama Tanzania ambayo kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ufundishaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe umepata msingi mzuri.

---

<sup>2</sup> Edwell Dzomba, Aaron A. Mukandabvute na Monica Davison.

## **2.0 Maendeleo ya Kiswahili nchini Zimbabwe baada ya Kutambulishwa Rasmi katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe**

Baada ya Kiswahili kutambulishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe, watu wengi walipata utambuzi wa umuhimu wa lugha hii. Juhudi za kukiendeleza Kiswahili nchini Zimbabwe zilianza kuonekana mwaka 2016 ambapo Wizara ya Elimu, chini ya Dkt. Lazarus Dokora, ilitangaza mtaala mpya wa shule za msingi na sekondari. Mtaala huo umeshapitishwa. Kinachosubiriwa ni maandalizi na utekelezaji wa mtaala huo. Ikiwa utekelezaji utafanyika, basi Kiswahili kitapata msukumo mpya. Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kigeni zilizotambulika kama lugha zitakazofundishwa katika shule za msingi mpaka sekondari. Lugha zingine zilizochaguliwa ni Kifaransa, Kichina na Kireno (Mashaire, 2016). Kutokana na changamoto mbalimbali kama upatikanaji wa walimu na rasilimali za kuanzisha ufundishaji wa Kiswahili, bado mchakato wa kufundisha Kiswahili unaendelea kuandaliwa. Chombo cha Ukuzaji Mitaala na Huduma za Kiufundi (*Curriculum Development and Technical Service*) kikishirikiana na Wizara ya Elimu kinaendelea kuandaa mazingira ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Zimbabwe. Juhudi za kuwezesha ununuaji wa vitabu vinavyohitajika katika ufundishaji zimeshaanza. Juhudi hizo zinahusisha viongozi wenye mamlaka serikalini kupata ushauri kutoka kwa walimu wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Zimbabwe.

Kwa mujibu wa Moyo (2017), Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kigeni zinazotarajiwa kufundishwa ili kuwaandaa wanafunzi kusoma katika mazingira ya kiutandawazi. Akimnukuu Afisa Mkuu wa Elimu nchini Zimbabwe, Bw. Sifiso Ndlovu, anaonesha kuwa walimu wa Zimbabwe wameshapokea uingizwaji wa Kiswahili katika elimu kwa sababu lugha kama hii itawawezesha wanafunzi kupata ujuzi katika nyanja mbalimbali. Mintarafu matarajio ya Kiswahili nchini Zimbabwe, tunaweza kusema ni makubwa kwa sababu watu wengi wameshapata utambuzi wa kujua umuhimu wa Kiswahili katika maendeleo ya nchi ya Zimbabwe. Wataalamu na wanazuoni kutoka shule na vyo mbalimbali nchini Zimbabwe wameshalipokea vizuri suala la ufundishaji wa Kiswahili. Kuna mambo mbalimbali ambayo yamesababisha Kiswahili kupokelewa na watu wengi nchini Zimbabwe. Baadhi ya mambo hayo ni biashara, elimu, siasa, teknolojia, na sanaa, kwa kutaja tu machache. Mambo haya, kwa namna moja au nyingine, ndiyo yamesababisha maendeleo ya Kiswahili kuwa yalivyo sasa nchini Zimbabwe. Kwa hiyo, ni vyema tuangalie maendeleo ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali ili tuweze kuwa na uelewa zaidi wa maendeleo ya Kiswahili nchini Zimbabwe.

### **2.1 Kiswahili na Teknolojia**

Katika karne ya kumi na tisa, ishirini, na ishirini na moja kumekuwa na maendeleo makubwa katika uwanja wa teknolojia duniani, yakiwamo mawasiliano, vyombo vya habari, elimu, usafiri na usafirishaji, na biashara. Maendeleo haya yamesababisha kuenea kwa Kiswahili duniani kupitia matumizi ya lugha ya

Kiswahili katika vyombo mbalimbali. Kwa kuangalia matumizi ya Kiswahili katika simu, ni wazi kwamba Kiswahili ni mojawapo ya lugha zilizoorodheshwa kuwa zinatumiwa katika simu za kiganjani (Mutembezi, 2011). Kupitia matumizi hayo ya simu, wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe wamepata uwezo wa kuweka kamusi za kielektroniki kwenye simu zao. Kamusi hizi hupatikana kirahisi katika programu ya *Google Playstore* na tovuti mbalimbali za mtandaoni. Mifano ya kamusi hizi ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (KKK) na *Kamusi ya Karne ya 21*. Jambo hili linawasaidia sana wanafunzi wakiwa darasani kwa sababu wanakuwa na uwezo wa kutafuta maana za maneno mbalimbali ya Kiswahili katika kamusi zao za simu za kiganjani. Kwa mantiki hiyo, tunaweza kuona kwamba matumizi ya Kiswahili katika simu za wanafunzi ni ishara inayoonesha kuwa Kiswahili ni lugha inayofundishika nchini Zimbabwe ikifungamana na maendeleo ya teknolojia. Kutokana na sifa ya kuwa lugha ya kiutandawazi, Kiswahili kimeonesha nguvu ya kuwa na sifa za lugha zinazotambulika kuwa zinaenea kwa kasi nchini Zimbabwe. Kwa hali ilivyo sasa, tunaweza kusema kwamba Kiswahili, kama Kiingereza, ni lugha ambayo imepiga hatua nchini Zimbabwe kwa kuwa na sifa zenye kuendana na mabadiliko katika teknolojia na matumizi ya vyombo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Moshi (2006), nguvu za Kiswahili katika maendeleo ya teknolojia zimebainika kupitia matumizi ya Kiswahili katika kampuni za mitandao ya simu za kiganjani. Makampuni kama *Vodacom*, *Airtel*, *Tigo* na zingine nchini Tanzania, yanatumia Kiswahili katika matangazo yake katika magazeti na sehemu mbalimbali. Lengo kuu hapa ni kuona kwamba wateja wa makampuni husika wanaelewa kinachotangazwa kupitia lugha yao na kufanikisha maendeleo ya biashara. Jambo hili halibaki kuwa la Afrika Mashariki tu bali kuna matangazo ya makampuni haya yanayooneshwa katika televisheni kupitia mashirika ya habari ya kimataifa kama DSTV na Kweze TV. Kwa kiasi fulani matumizi ya Kiswahili katika matangazo hayo yanawaathiri Wazimbabwe katika kujifunza lugha ya Kiswahili na kuona kuwa ni lugha inayowezekana kufundishwa.

Isitoshe, katika teknolojia Kiswahili ni lugha ambayo imetambuliwa na *Microsoft* kwa kiasi kikubwa. Jambo hili lilisababisha kutengenezwa kwa programu ya kielektroniki (*Optical Character Recognition Software - OCRS*) inayotambua matini za Kiswahili. Kwa mujibu wa gazeti la *Majira* (2004) kama linavyonukuliwa na Moshi (2006), sababu za *Microsoft* kuchagua Kiswahili ni kwamba ni lugha yenye nguvu za kusimamia maendeleo duniani na vilevile ni lugha ya kibiashara. *Microsoft* haikuishia hapo, iliendelea kutambua Kiswahili kupitia kuanzisha na kuitambulisha programu inayomwezesha mtumiaji wa kompyuta kuiweka kwenye kompyuta yake yaani *Microsoft Kiswahili Proofing Tools* na baadaye kuitumia kuhariri makosa ya kiuandishi katika matini za Kiswahili. Kwa hivi sasa, wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe wanatumia teknolojia hii katika kazi zao na jambo hili linakuza ufanisi wao wa lugha ya Kiswahili. Kwa kuangalia mifano hii, tunaona kwamba kutokana

na maendeleo ya teknolojia, hali ya Kiswahili nchini Zimbabwe inaonesha matumaini makubwa ya kuenea katika nchi nzima.

## **2.2 Kiswahili na Sanaa**

Kiswahili ni mojawapo ya lugha ambazo zimeshika kasi kimatumizi katika nyanja mbalimbali za sanaa, kwa mfano, katika filamu, michezo ya kuigiza, muziki na kadhalika. Katika filamu, inatambulika kuwa filamu za Bongo (*Bongo Movies*) zimevuka mipaka duniani. Kutokana na maendeleo katika teknolojia, filamu hizi zinaoneshwa kwenye televisheni pamoja na mtandaoni, hususani *YouTube*. Filamu nyingi za Bongo (Tanzania) zinatumia Kiswahili na baadhi huwekwa maandishi ya Kiingereza chini ya picha kama njia ya kutafsiri yale yanayosemwa na kuigizwa katika filamu hizo. Jambo hili limewafanya Wazimbabwe wanaojua Kiingereza kupata fursa ya kujua maneno machache ya Kiswahili yanayotafsiriwa katika Kiingereza. Kwa hiyo, siku hizi suala la kutojua lugha ya Kiswahili siyo kikwazo tena katika kufurahia filamu za Bongo nchini Zimbabwe. Watu wanakuwa na uwezo wa kujua yanayoendelea katika filamu kupitia tafsiri zinazowekwa na hivyo kujua maana ya maneno yanayosemwa katika Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili imeshavuka mipaka ya Afrika Mashariki katika sanaa ya muziki. Wanamuziki wengi nchini Zimbabwe wamekichangamkia Kiswahili kuwa lugha ya sanaa. Aidha, kuna kazi kadhaa za wanamuziki wa Kiswahili kutoka Afrika Mashariki zinazorushwa nchini Zimbabwe katika redio na televisheni. Tunaweza pia kuangalia mifano kutoka muziki wa Bongo Flewa. Mwaka 2016, mwanamuziki maarufu Nasibu Abdul Juma (Diamond Platnumz) wa Tanzania alishirikiana na Mukudzeyi Mukombe (Jah Praizah) ambaye ni mwanamuziki maarufu nchini Zimbabwe. Wimbo wao uitwao *Watora Mari* (Umechukua Pesa) umekuwa maarufu sana siyo nchini Zimbabwe na Tanzania tu bali pia ulienea mpaka Marekani na Ulaya. Wimbo huu ni mchanganyiko wa lugha za Kishona na Kiswahili. Wanamuziki hawa walionesha mwanga katika uhusiano uliopo baina ya lugha hizi mbili ambazo ni za Kibantu. Walionesha kuwa siyo vigumu kwa mtu azungumzaye Kiswahili ama Kishona kuwa na ufanisi wa kujua lugha zote mbili na kuzibadilisha wakati wa kuongea. Kuonesha hali ya Kiswahili kuwa ni lugha yenye matumaini makubwa nchini Zimbabwe, mwanamuziki Jah Praizah miaka miwili baada ya kufanya kazi pamoja na Diamond, alitoa wimbo mwingine mpya unaoitwa *Ronika* ambao unabeba maneno ya Kiswahili, kwa mfano, ‘kidogokidogo’. Jambo hili linaonesha hali ya Kiswahili nchini Zimbabwe kuwa ni lugha yenye uwezo wa kuenea katika nchi nzima.

Katika sanaa ya muziki, Kiswahili kimeshika nafasi inayoonesha ishara ya maendeleo kwa kiasi fulani. Wanamuziki wengine wametumia majina ya Kiswahili kubainisha makundi yao na kuyatofautisha na makundi mengine. Kwa mfano, mwanamuziki maarufu wa aina ya muziki unaoitwa *Museve* (Mshale), Aleck Macheso, amelipa kundi lake jina la Sungura Band. Kama tulivyoonesha awali, jina hili limekuwa maarufu sana nchini Zimbabwe ila cha kushangaza ni



kwamba, ni watu wachache sana wanaojua maana ya jina sungura. Hata hivyo, watu wengi hawajui kuwa Sungura ni jina la Kiswahili ambalo lina maana ya Tsuro<sup>3</sup>. Matumizi ya Kiswahili katika sanaa ni ishara inayoonesha dalili nzuri katika kukiendeleza Kiswahili katika nchi ya Zimbabwe.

Baada ya wimbo uitwao “Nakwenda Zimbabwe” wa Ibrahim Mussa (Roma Mkatoliki) wa mwaka 2017 kuwa maarufu sana katika nchi ya Tanzania na nchi mbalimbali za Afrika, wasanii wa Zimbabwe nao hawakubaki nyuma katika kuliimbia taifa lao. Wimbo wa Roma ulikuwa maarufu katika vyombo vya habari kama redio na televisheni, mitandao ya kijamii kama *Facebook*, *WhatsApp* na *YouTube*. Mwezi Januari mwaka 2018, mwanamuziki wa Zimbabwe anayeitwa Resilience Chekera (Gze) alitoa wimbo unaoitwa *Gaya Zimbabwe*<sup>4</sup>. Katika wimbo huu, alichukua sauti kutoka wimbo wa Roma Mkatoliki hususani kwenye kiitikio wanapoimba kwamba ‘nakwenda Zimbabwe’ akachanganya na maneno ya lugha ya Kishona. Ingawa si lengo la makala hii kuelezea suala la utaifa lakini kuchanganywa kwa lugha hizi mbili, Kishona kutoka Afrika Kusini na Kiswahili kutoka Afrika Mashariki kunaonesha mahusiano mazuri baina ya lugha hizi mbili. Hivyo, ni kusema kwamba, katika nchi ya Zimbabwe Kiswahili kinapokelewa vizuri na kinapata fursa na mazingira mazuri ya kuenea kwa sababu kina mahusiano na lugha zinazozungumzwa katika nchi ya Zimbabwe.

### **2.3 Kiswahili na Siasa**

Novemba mwaka 2017 ni mwezi ambao Wazimbabwe wengi waliuona kama wa mabadiliko katika siasa za nchi ya Zimbabwe. Aliyekuwa rais wa nchi hii kwa miaka zaidi ya 36, Rais Robert Gabriel Mugabe, aliondolewa madarakani. Katika kuhitimisha hotuba yake aliyotoa tarehe 19 Novemba 2017, alimalizia kwa kusema ‘Asante Sana’. Utumiaji wa Kiswahili uliwashangaza raia wengi na maneno haya ya Kiswahili yalichukua nafasi kubwa katika mijadala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kielimu. Maneno haya yalitumika sana, kwa mfano, katika mitandao ya kijamii kama *Twitter*, *Facebook* na *WhatsApp*. Wazimbabwe wengine walikuwa wanajua maana ya maneno haya na wengine hawakuyajua, wakayatafuta. Aidha, wengine walikuwa wanayatumia tu bila kujua wanachomaanisha ni nini (Dzomba, 2018). Lengo la kazi hii si kuchunguza sababu za Mugabe kutumia maneno haya ya Kiswahili, lakini kutokana na mfano huu tunaona kuwa kupitia matumizi ya Kiswahili kwa viongozi nchini Zimbabwe, Kiswahili kinaonesha maendeleo mazuri na uwezo wa kuenea kwa kasi sana nchini humo. Aidha, jambo hilo la kutumia Kiswahili kwa Mugabe halikuwa jipya. Januari 2016, Mugabe alishiriki katika uchapishaji wa kitabu cha kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kitabu hiki kinaitwa *Julius Nyerere, Asante*

---

<sup>3</sup> Sungura katika lugha ya Kishona.

<sup>4</sup> Maana yake kwa Kiswahili ni Fikiria Zimbabwe.

*Sana Thank You Mwalimu* (Herald, January 2016)<sup>5</sup>. Ingawa Mugabe alipata maarifa ya kuzungumza Kiswahili katika kipindi cha vita vya kupigania uhuru alipoishi Tanzania, kutumia kwake Kiswahili baada ya miaka mingi kunaonesha kwamba alikijali na alikuwa na imani kwamba lazima kuna wananchi wake wanaomwelewa.

### 3.0 Matarajio ya Kiswahili Nchini Zimbabwe

Pamoja na kuwa lugha ya kimataifa, Kiswahili ndiyo lugha ambayo inaweza kutumika katika juhudi za umajumui wa Afrika. Kiswahili ni lugha ya Waafrika, kwa hiyo, katika kuliweka bara la Afrika katika nafasi nzuri ya maendeleo, lazima Kiswahili kitumike katika nyanja mbalimbali, mathalani, biashara, elimu, sanaa, siasa, kutaja tu kwa uchache. Hili ndilo jambo ambalo Wazimbabwe wamelitambua na kuona umuhimu wa kukichangamkia Kiswahili katika kushirikiana na Waafrika wengine katika maendeleo. Isitoshe, uchangamkiaji wa kukifundisha Kiswahili katika nchi ya Zimbabwe ni ishara inayoonesha kuwa kutokana na hali ilivyo sasa, Waafrika wameshakitambua Kiswahili kama lugha ya maendeleo ya Afrika. Hii ni mojawapo ya juhudi za kuondoa vikwazo vya mawasiliano baina ya nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika. Hivyo, matarajio ya nchi kama Zimbabwe katika Kiswahili ni kuona kuona kwamba lugha ya Kiswahili inakuwa chombo cha kuondoa mipaka iliyowekwa na wakoloni na vilevile kuwaunganisha Waafrika kuwa pamoja. Nchi ya Zimbabwe haiko karibu na bahari, kwa hiyo, inategemea nchi kama Tanzania kupokea mizigo inayotoka mabara mengine. Hivyo, kuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa Wazimbabwe wengi kutafaa zaidi katika kuendeleza biashara zao.

Pia, ni dhahiri kwamba sifa za lugha ya Kiswahili ni msukumo mwingine wa ukuaji wa lugha hii kwa haraka sana katika nchi ya Zimbabwe. Kiswahili na Kishona ni lugha za Kibantu na kuna baadhi ya maneno ambayo yanafanana kitahajia, utamkaji na maana, kama Jedwali Na. 1 lifuatalo linavyoonesha:

#### Jedwali Na. 1: Maneno Yanayofanana katika Kishona na Kiswahili

Kiswahili	Kishona
Nyoka	Nyoka
Ngoma	Ngoma
Baba	Baba
Imba	Imba
Moto	Moto

**Chanzo:** *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013) na Chimhundu (2001)

Maneno yanayoonekana katika Jedwali Na. 1 ni kwa uchache tu lakini kuna baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo yanafanana kwa kiasi kikubwa na maneno ya

<sup>5</sup> Gazeti la mtandaoni la Zimbabwe.

lugha ya Kishona. Jambo hili ni mojawapo ya ishara inayoonesha kuwa matamano ya kujifunza Kiswahili nchini Zimbabwe ni makubwa kwa sababu kujifunza lugha ya Kiswahili haitakuwa kazi ngumu kwa Wazimbabwe kutokana na maneno yanayofanana katika lugha hizo mbili.

Matamano haya yataweza tu kutimizwa iwapo mahitaji mengi ya kukitumia Kiswahili yanayojitokeza katika siasa, elimu, vyombo vya habari na biashara yatatimizwa ili Wazimbabwe wote wapate utambuzi kuhusiana na umuhimu wa Kiswahili. Sehemu inayofuata inaeleza nini kifanyike ili kutimiza mahitaji ya uendelezaji wa Kiswahili katika nchi ya Zimbabwe.

#### **4.0 Mahitaji**

Kuna mambo kadhaa ambayo yanahitajika ili kukiendeleza Kiswahili nchini Zimbabwe. Katika kipengele hiki tutaangalia mahitaji katika nyanja mbalimbali kwa mfano elimu, siasa, biashara, na vyombo vya habari.

#### **4.1 Mahitaji katika Elimu**

Kama tulivyoonesha hapo awali, hivi sasa Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kigeni zinazotambulika katika mfumo wa elimu wa Zimbabwe. Kiswahili kiliingizwa katika mtaala mpya wa elimu ya Zimbabwe ili kifundishwe kama somo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari. Mpaka sasa, jambo hilo halijatekelezwa kutokana na kukosekana kwa vitu mbalimbali. Kwa hivi sasa walimu wanaofundisha Kiswahili ni wachache sana na hakuna shule ya msingi wala sekondari inayofundisha Kiswahili. Jambo hili limesababisha changamoto mbalimbali hususani kwa wale wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya tatu katika ngazi ya shahada ya kwanza. Wanafunzi wanaoanza kujifunza lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe wanakumbana na changamoto nyingi kwa sababu wanakuwa hawana msingi mzuri wa lugha hii. Kwa hiyo, ni vyema wizara ya elimu itekeleze suala la ufundishaji wa Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi sekondari ili wanafunzi wanapofika chuoni wawe na msingi mzuri. Vilevile, walimu wa Kiswahili waongezewe vitabu mbalimbali vinavyotumika kufundishia Kiswahili.

Isitoshe, vyo vikiu kama vile cha Zimbabwe ambapo Kiswahili kinafundishwa, viwe na wajibu wa kuwa mfano katika kuonesha mwanga katika umuhimu wa Kiswahili. Kabla ya kuwadahili wanafunzi wa Kiswahili ni vyema kuwatembelea kwanza katika shule za msingi na sekondari na kuwafundisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili ili wanapofika ngazi ya digrii wawe na utambuzi wa kujua umuhimu wa lugha wanayosoma. Jambo jingine linalohitajika ni ushirikiano baina ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili nchini Zimbabwe na wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Afrika Mashariki. Wanafunzi wanaosoma Kiswahili nchini Zimbabwe wakipata fursa ya kushirikiana na shule mbalimbali za Afrika Mashariki, watakuwa na uelewa mzuri kuhusu lugha ya Kiswahili.

Kutokana na jambo hili wanafunzi hao hawatajifunza lugha tu bali hata utamaduni wa Waswahili, hivyo, wataweza kuuelewa vyema kuliko kuusikia tu darasani.

#### **4.2 Mahitaji katika Siasa**

Viongozi wa kisiasa wanaweza kukitumia Kiswahili ili kuonesha umuhimu wake katika nchi ya Zimbabwe. Kama tulivyoonesha hapo awali kwamba Kiswahili siyo lugha ambayo tunaweza kusema ni ngeni, kabla ya kuanza kufundishwa rasmi ilikuwa katika nyanja mbalimbali nchini Zimbabwe. Kuna wanajeshi wa Zimbabwe walioishi katika kambi za Morogoro, Bagamoyo na Nachingwea nchini Tanzania katika kipindi cha vita vya kupigania uhuru. Wanajeshi hawa wanaongea Kiswahili na wengine wameshajiunga na siasa. Kama viongozi wa siasa ni vyema wakachangamkia nafasi hii katika kuwapatia raia utambuzi wa umuhimu wa Kiswahili katika kuwaweka pamoja Waafrika.

Aidha, viongozi wa siasa wawe na kazi ya kuwaonesha raia umuhimu wa Kiswahili katika maendeleo ya nchi za Kiafrika. Mathalani, mwaka 2004 katika Mkutano wa Umoja wa Afrika ambapo aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Joachim Chissano, aliwahutubia kwa Kiswahili washiriki ambao wengi walikuwa ni marais (Babaci-Wilhite, 2013). Isitoshe, aliyekuwa Rais wa Naijeria, Olusegun Obasanjo, alifuata nyayo za wapigania Kiswahili kwa kuwasalimia marais akitumia Kiswahili katika kongamano la Umoja wa Nchi za Kiafrika la African Union (AU) mwaka 2005 (Moshi, 2006). Kwa kuangalia mifano hii tunaona kuwa viongozi wa siasa na serikali ya nchi ya Zimbabwe wanaweza kuchangia kwa asilimia kubwa katika kukieneza Kiswahili nchini. Viongozi hawa wana nafasi ya kuwaelimisha wanajamii kuhusu umuhimu wa Kiswahili kwa raia wote na kuwaonesha faida za kukijua Kiswahili ili waweze kuwa na mahusiano na nchi za Afrika Mashariki.

#### **4.3 Mahitaji katika Biashara**

Kama tulivyoonesha awali kwamba sehemu kubwa ya bidhaa za biashara zinazouzwa nchini Zimbabwe zinaingia kupitia bandari ya Dar es Salaam ya Tanzania, wafanyabiashara wengi wanaotembelea sehemu hiyo wanakumbana na changamoto za kimawasiliano. Ni vyema wizara inayoshughulika na mambo ya uchumi kutengeneza taasisi zinazoshughulika na suala la ufundishaji wa Kiswahili kwa wafanyabiashara ili kuondoa vikwazo vya kimawasiliano. Aidha, ni vyema pia wafanyabiashara kujiunga na kozi za muda mfupi, kwa mfano *Kiswahili katika ngazi ya awali* zinazofundishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Kozi kama hizi zitawasaidia kuwa na msingi mzuri wa lugha ya Kiswahili na kufanya biashara zao bila vikwazo vya kimawasiliano.

#### **4.3 Mahitaji katika Vyombo vya Habari na Sanaa**

Kama tulivyoonesha hapo juu, ni katika vyombo vya habari kama redio, magazeti pamoja na televisheni ambapo uelewa wa lugha unaweza kupatikana. Redio za

Zimbabwe, kwa mfano, National FM ambayo inatumia lugha mbalimbali za Kibantu, zifanye kazi ya kukitumia pia Kiswahili katika vipindi vyake ili watu wapate utambuzi katika umuhimu wa Kiswahili. Magazeti yanaweza kutenga nafasi ndogo kwa ajili ya somo la lugha ya Kiswahili la kila siku au la wiki. Jambo hili litawashawishi raia wengi wa Zimbabwe kukichangamkia Kiswahili na kushirikiana na Waafrika wengine katika kuieneza lugha ya umajumui.

Akijadili kuhusu Kiswahili katika muziki wa Tanzania, Sekella (1995) anaeleza kwamba katika suala la kuelimisha watu, muziki humfanya mtu ajenge kumbukumbu ya vitu au tukio kwa urahisi na kumbukumbu hiyo huweza kudumu kwa muda mrefu. Ingawa Sekella (1995) alizungumzia muziki wa Kiswahili kwa Watanzania, siyo jambo baya Wazimbabwe kujifunza Kiswahili na kuweza kupokea elimu na mawazo yanayowasilishwa katika muziki wa Watanzania kama wanavyozifurahia na kuelimishwa na nyimbo kutoka lugha zingine kama Kiingereza. Aidha, ni kazi ya wanamuziki wa Zimbabwe pia kusoma na kutunga muziki wa Kiswahili ili waweze kupata soko la Afrika Mashariki; hili ni jambo linaloweza kuleta mafanikio katika kazi zao. Kwa hiyo, Kiswahili ni lugha ambayo inahitajika katika kuendeleza sanaa na maisha ya wasanii nchini Zimbabwe.

## **5.0 Hitimisho**

Kwa kuhitimisha, Kiswahili ni lugha ambayo imeenea sana duniani na matokeo yake ni makubwa katika juhudi za maendeleo barani Afrika. Kuanzishwa kwa ufundishaji wa Kiswahili nchini Zimbabwe ni mojawapo ya ishara za maendeleo ya Kiswahili duniani na vilevile ni ishara inayoonesha hali ya Kiswahili kama lugha yenye uwezo wa kuwaunganisha Waafrika bila vikwazo vya mipaka vilivyowekwa na wakoloni. Nchi ya Zimbabwe imekuwa na Kiswahili katika nyanja mbalimbali na si kweli kwamba kuanzishwa kwa ufundishaji rasmi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe ndiyo mwanzo wa Kiswahili katika nchi hiyo. Kiswahili kilikuwapo lakini watu walikuwa hawajapata utambuzi wa kujua umuhimu wake. Katika makala hii tumeleza historia ya Kiswahili kabla ya kuanzishwa katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Tumefafanua pia mchakato wa kutambulishwa kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe na kuangalia hali yake katika nyanja mbalimbali. Tumehitimisha kwa kuonesha kuwa Kiswahili kinaweza kuenezwa nchini Zimbabwe iwapo mahitaji ya kukitumia yanayojitokeza katika siasa, vyombo vya habari na sanaa, elimu na biashara yatatimizwa.

## **Marejeleo**

- Chimhundu, H. (2001). *Duramazwi Guru reChishona*. Harare: College Press.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1997). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Babaci-Wilhite, Z. (2013). Local Languages of Instruction as a Right in Education for Sustainable Development in Afrika, *Journal of Sustainability*, 5: 1994-2017.

- Dzomba, E. (2018). "Revising the meaning of Asante Sana: The Role of Social Media in the Development of Kiswahili in Zimbabwe", The Paper presented at the International Conference on Social Media, University of Zimbabwe.
- Karangwa, J. D. (2006). Kiswahili katika Karne ya 20: Chombo cha Ukombozi, Utaifa na Ukandamizaji, *Kioo cha Lugha*, 4: 62-72.
- Kezilahabi, E. (1983). Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili, *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 145-165.
- Massamba, D. P. B. (2008). *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence - Convergence Theory*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- \_\_\_\_\_. (2002). *Historia ya Kiswahili 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mashaire, M. (2016). Mandarin, Swahili in New Curriculum, *Herald*. 01.06.2016 <http://www.herald.co.zw/mandarin-swahili-in-new-curriculum/imesomwa-tarehe-10-Januari,-2018>.
- Mazrui, A. M. na Shariff, I. N. (1994). *The Swahili: Idiom and Identity of an African People*. Africa. Trenton: World Press.
- Moshi, L. (2006). "The Global World languages: The Case of Kiswahili," in Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics, ed. Olaoba F. Arasanyin and Michael A. Pemberton, pgs.166-175. University of Georgia.
- Moyo, T. (2017). Pupils to learn Mandarin, Swahili, *Herald*. 18.01.2017 <http://www.herald.co.zw/pupils-to-learn-mandarin-swahili/> imesomwa tarehe 27 Agosti, 2018.
- Mulokozi, M. M. (2003). Kiswahili as a National and International Language, *Kiswahili*, 66: 66-80.
- Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A Case of Uganda, *Nordic Journal of African Studies*, 15(2):154-165.
- Mutembei, A. K. (2011). Kukitandawazisha Kiswahili Kupitia Simu za Kijanjani: Tafakari Kuhusu Isimu Jamii, *Swahili Forum*, 18:198-210.
- Nurse, D. and Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African People*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Sekella, M. (1995). Kiswahili katika Muziki wa Tanzania, *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Timmamy, R. na Swaleh, A. (2016). Ulimwengu wa Kanga, *Journal of Language and Linguistics*, 5:195-203.
- TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.